



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

**MKUTANO WA KUPOKEA MAONI YA WADAU KUHUSU UTARATIBU WA
MATUMIZI YA MITA ZA KUKOKOTOA NAULI ZA TEKSI ZA KAWAIDA -
JUMATANO, TAREHE 14 DISEMBA 2022 KATIKA UKUMBI WA
ANATOUGLOU, DAR ES SALAAM**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawaalika wadau wa huduma za usafiri wa tekisi kuhudhuria mkutano wa kupokea maoni ya wadau, kuhusu utekelezaji wa matumizi ya mita za kukokotoa nauli za usafiri wa tekisi (Cabs), utakaofanyika **Jumatano, tarehe 14 Disemba 2022 katika Ukumbi wa Anatougrou, kuanzia saa 3.00 asubuhi.**

Kanuni ya 15(d) ya Kanuni za Usafiri wa Kukodi za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za 2020, zinaelekeza kuwa, Leseni ya Usafiri wa Kukodi itatolewa kwa chombo kilichounganishwa na mita ya kukokotoa nauli au mfumo mwingine unaoweza kukokotoa nauli kama itakavyoamuliwa na Mamlaka.

Kwa mujibu wa kifungu cha 21(2)(b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, Mamlaka inapaswa kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa masuala ya kiushindani katika huduma zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa matumizi ya mita za kukokotoa nauli za usafiri wa tekisi.

Aidha, LATRA itapokea maoni kwa njia ya maandishi kutoka kwa wadau wa usafiri wa tekisi za kawaida. Maoni hayo yataanza kupokelewa kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe 28 Disemba, 2022 kupitia anwani zifuatazo;

**Mkurugenzi Mkuu,
LATRA Makao Makuu,
S.L.P. 1742, 41104 Tambukareli
DODOMA, TANZANIA.**
Baruapepe: info@latra.go.tz na dg@latra.go.tz

**Imetolewa na:
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano – LATRA
30 Novemba, 2022**